*Picha ya Kwanza juu, kushoto ni Mrs. Mbogo (Salome), kulia ni Mr. Mbogo na Jayden*



*Picha zinazofuata zinaonesha washirika wakiwa katika ibada niliyoshiriki. Picha mbili kutoka kulia zinaonesha nikishiriki nao kupima msingi wa jengo la kanisa tayari kwa kazi ya ujenzi, na picha ya chini kushoto ni jengo la kanisa baada ya ujenzi kukamilika.*

Kwa maelezo yao, walisema kwamba walikuwa wanafuata huduma ya ibada kijiji cha jirani ambapo ilikuwa ni umbali mrefu sana hasa ukizingatia miongoni mwao walikuwamo wazee na watoto pia. Hivyo, wakaamua kujenga banda la muda la kufanyia ibada na hadi nawatembelea ilikuwa yapata kipindi cha zaidi ya miaka mitatu iliyopita toka waanzishe huduma ya ibada mahali hapo. Muujiza wao mkubwa ilikuwa ni pale walipopata msaada wa kununuliwa turbai kwa ajili ya kuwakinga na jua pamoja na mvua. Hata wakati huo waliniomba kama nitaweza niwanunulie turbai kabla msimu wa mvua haujaanza.